JARIDA LA TOLEO 05 12/08/2021

# UFUNDI STADI

# WAZIRI MKUU MAJALIWA AGUSWA NA MCHANGO WA PROF. MWANDOSYA KATIKA UFUNDI STADI



PG 4 MHAGAMA ATAKA KIPAUMBELE CHA MIKOPO KIWE KWA WENYE UFUNDI STADI

PG 8 WAKULIMA 2,176 NCHINI WANUFAIKA NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

PG 12 VETA YAKABIDHI VIFAA VYA MILIONI 62 KWA VYUO BINAFSI

PG 15 CHUO KIPYA CHA VETA KUANZISHWA WANGING'OMBE



# WAZIRI MKUU MAJALIWA AGUSWA NA MCHANGO WA PROF. MWANDOSYA KATIKA UFUNDI STADI

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa ameeleza kuguswa na mchango wa Prof. Mark Mwandosya katika kuwezesha utoaji mafunzo ya ufundi stadi mkoani Mbeya kwa kuipa serikali majengo aliyokuwa akiyamiliki ili yabadilishwe na kuwa chuo cha ufundi stadi.

Mwaka 2017, Prof. Mwandosya na familia yake walitoa majengo yaliyokuwa ya kituo chao cha kulelea watoto yatima cha 'Lucy Hope Centre' na kuyakabidhi kwa VETA ili kuanzisha chuo cha ufundi stadi.

Akizindua Chuo cha VETA Busokelo tarehe 1 Agosti 2021, Mhe. Majaliwa alimshukuru Profesa Mwandosya na familia yake kwa kitendo hicho cha kizalendo na kueleza kuwa Chuo hicho kitasaidia sana vijana wa Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo na maeneo mengine mkoani Mbeya kujipatia ujuzi na kuanzisha shughuli zao mbalimbali za kiuchumi...

"Jambo mlilolifanya si jambo dogo na wala siyo jambo rahisi kwa watu wengine ila ni kwa watu wenye maono ya mbali na mapenzi mema... Mlichokifanya hakitasahaulika na hatuna namna ya kuwashukuru wala fedha ya kuwalipa kufidia kwa jambo hili, bali shukrani zetu ni kuendelea kuiheshimu familia ya Prof. Mwandosya," alisema Majaliwa



Mhe. Majaliwa alitumia fursa hiyo kuwasihi vijana wa Busokelo waliopata fursa ya ufadhili wa Serikali kupitia programu maalumu ya mafunzo ya ufundi stadi kwa ufadhili wa Ofisi yake watumie vizuri fursa hiyo ili wanufaike.

Alisema zaidi ya vijana 45,000 wanaendelea na mafunzo katika vyuo vya ufundi stadi nchini ili wajipatie ujuzi kwenye maeneo mbalimbali kwa miezi sita ambapo Serikali imelipia ada ya mafunzo kwa asilimia 100.



Awali, Mkurugenzi Mkuu wa VETA Dkt. Pancras Bujulu alisema chuo hicho kina uwezo wa kudahili wanafunzi 120 kila mwaka kwa kozi za muda mrefu na 320 kwa kozi za muda mfupi kwa mwaka.

Alisema kupitia programu ya ufadhili wa Ofisi ya Waziri Mkuu, chuo cha VETA Busokelo kimedahili wanafunzi 127 katika fani za Useremala, Ushonaji, Umeme wa Majumbani, ukarabati wa Vitarakimishi (Computer Maintanance) na Utengenezaji wa vifaa vya kielektroniki.



> Tumeongeza vyuo vya Ufundi VETA na nimeona VETA kwenye maonesho na nimeona kazi yao nzuri wanayofanya. VETA tuliokuwa tunaifahamu miaka kama 10 nyuma sio VETA ya sasa hivi, sasa hivi tunafanya vizuri zaidi,

**MHE. SAMIA SULUHU HASSAN**
RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

*SIKU YA KIMATAIFA YA WANAWAKE NA WASICHANA KATIKA SAYANSI TAREHE 11 FEBRUARI 2021*



## MHAGAMA ATAKA KIPAUMBELE CHA MIKOPO KIWE KWA WENYE UFUNDI STADI

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Mhe. Jenista Mhagama, amewataka viongozi wa mikoa na halmashauri nchini kutoa kipaumbele cha mikopo kwa wahitimu wa ufundi stadi ili kuwawezesha kujiajiri na kuajiri wengine.

Waziri Mhagama ameyasema hayo Jumamosi, tarehe 31 Julai, 2021, alipotembelea na kukagua shughuli za utekelezaji wa programu ya mafunzo ya Uanagenzi inayofadhiliwa na Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu katika Chuo cha VETA Busokelo, Wilaya ya Rungwe, mkoani Mbeya.

“Nawaomba sana viongozi wa mikoa na halmashauri mtoe kipaumbele cha mikopo kwa kwa hawa vijana ili wapate mitaji na vifaa vya kufanyia kazi baada ya kuhitimu. Tena ukiwapa hawa watachangia kuongeza mapato kwenye halmashauri yako na unakuwa na uhakika wa mikopo yako kurejeshwa, maana tayari wana ujuzi,” amesema.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), Dkt. Pancras Bujulu, ameishukuru Serikali kwa kuendelea kuwezesha vijana kupata mafunzo ya ufundi stadi na ameahidi kuwa Mamlaka itahakikisha vijana hao wanapata mafunzo bora yatakayowawezesha kujiajiri baada ya kuhitimu.



Akisoma taarifa ya utekelezaji wa programu hiyo katika Chuo cha VETA Busokelo, Kaimu Mkuu wa Chuo hicho, Bw. Wilbert Bendera, amesema jumla ya vijana 173 wa Halmashauri ya Busokelo walipata fursa ya mafunzo hayo katika fani za Useremala, Ushonaji, Umeme, Matumizi na Ukarabati wa Kompyuta na Utengenezaji Vifaa vya Kielektroniki, ingawa hadi sasa walioripoti ni 127 tu, sawa na asilimia 74.
Kufuatia taarifa hiyo, Waziri Mhagama ameagiza uongozi wa Chuo hicho kushirikiana kwa karibu na Mbunge wa Jimbo la Busokelo, Uongozi wa Halmashauri ya Busokelo, pamoja na Diwani wa Kata ya Lufilyo kuhakikisha nafasi za vijana ambao hawakuripoti zinajazwa mara moja ili wana-Busokelo wanufaike na fursa hiyo.



# MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

VOCATIONAL EDUCATION AND TRAINING AUTHORITY
VETA
SKILLED LABOUR FORCE - THE FUTURE OF TANZANIA

## TANGAZO LA NAFASI ZA MAFUNZO YA UFUNDI STADI KWA KOZI ZA MUDA MREFU KWENYE VYUO VYA VETA MWAKA 2022






MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (VETA) INAWATANGAZIA WANANCHI WOTE KUWA FOMU ZA MAOMBI YA MAFUNZO YA UFUNDI STADI YA MWAKA MMOJA HADI MIAKA MITATU KATIKA VYUO VYA VETA KWA MWAKA 2022 ZIMEANZA KUTOLEWA.

FOMU ZINAPATIKANA KATIKA VYUO VYOTE VYA VETA NCHINI NA KWENYE TOVUTI YA VETA www.veta.go.tz

KUANZIA TAREHE 2 AGOSTI HADI 15 SEPTEMBA 2021.

**Kwa Mawasiliano**
**Baruapepe: info@ veta.go.tz**
**Simu: 0755 267 489**

KARIBU UJIUNGE NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA
MKURUGENZI MKUU
MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI - VETA

# MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

## TAARIFA KWA UMMA

## MAKAO MAKUU YA VETA KUHAMIA DODOMA

Julai 16, 2021

Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) inautangazia umma kuwa ofisi za VETA Makao Makuu zitahamishiwa rasmi katika Makao Makuu ya Serikali jijini Dodoma kuanzia tarehe 19 Julai, 2021.

Ofisi za Makao Makuu ya VETA zitahamia kwenye Jiji la Dodoma mtaa wa Mbugani, Barabara ya VETA, kwenye Jengo la Kiwanda cha Samani cha VETA pamoja na jengo lililokuwa la ofisi za VETA Kanda ya Kati. Anuani mpya ya VETA Makao Makuu itakuwa kama ifuatavyo;

VETA Makao Makuu,
Plot No. 18, Central business Park (CBP)
Barabara ya VETA,
S.L.P 802,
DODOMA.

Kwa Mawasiliano
Baruapepe: info@veta.go.tz
Simu: +255 26 2963661
Tovuti: www.veta.go.tz

Imetolewa na
Mkurugenzi Mkuu VETA
Julai 16, 2021



# WAKULIMA 2,176 NCHINI WANUFAIKA NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

Jumla ya wakulima 2,176 (wanawake 1,294 na wanaume 882) wa mikoa ya Morogoro, Iringa na Njombe wamenufaika na mafunzo ya stadi katika kilimo  na ufugaji yaliyotolewa kupitia mradi wa Tajirika na Kilimo unaotekelezwa na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), Shirika la Kimataifa la CARE na Taasisi ya Ukuzaji Kilimo Uwanda wa Kusini mwa Tanzania (SAGCOT).

Akizungumza wakati wa kikao cha tathmini ya utekelezaji wa mradi jijini Dodoma, tarehe 22 hadi 23 Julai 2021, Mratibu wa Mradi huo kutoka VETA, Bw. Perecy Ugula, amesema wakulima hao walipatiwa mafunzo ya ufugaji bora wa mifugo hasa ng'ombe wa maziwa na kuku, kilimo cha mazao mchanganyiko, na kilimo cha mbogamboga na matunda, na kufanikiwa kubadili uendeshaji wa shughuli zao hizo kuwa za kisasa na za kibiashara.

Kwa mujibu wa Bw. Ugula, mafanikio mengine yaliyopatikana kwenye mradi huo ni pamoja na uandaaji wa mitaala miwili ya sekta ya Kilimo, ambayo ni Mtaala wa Kilimo cha Mbogamboga na Matunda, Mtaala wa Kilimo cha Mazao, na kuuboresha mtaala wa Afya na Ufugaji wa Mifugo.

Kwa upande wake, Afisa Tathmini na Ufuatiliaji wa Shirika la Kimataifa la CARE, Bw. Edwin Sallu, amesema kupitia utekelezaji wa mradi huo wamegundua uwepo wa uhitaji mkubwa wa mafunzo ya stadi za kuboresha shughuli za kilimo kwa wakulima wadogowadogo vijijini na kwamba wengi wao wako tayari kugharamia mafunzo hayo kama inavyofanyika sasa katika Mradi wa Tajirika na Kilimo, hivyo akaiomba VETA kupanua zaidi wigo wa mafunzo kwa mfumo wa kuwafuata wahusika katika maeneo yao vijijini.

Sallu amesema mafunzo hayo yamewezesha kuunda vikundi 141 vya uzalishaji katika sekta ya kilimo cha mazao mchanganyiko, Mbogamboga na matunda na ufugaji wa kibiashara, ambapo kwa sasa wanafanya shughuli zao za kilimo kwa umoja, hali inayowezesha uzalishaji mazao kwa wingi, ubora na uhakika wa kufikia masoko ya bidhaa zao na kuwezesha wakulima hao kukopesheka kwa urahisi na kupata faida nzuri.

"Kwa kweli tumeshuhudia manufaa makubwa ya mafunzo yaliyotolewa kupitia mradi huu kwa wakulima...



vijijini, hasa ukizingatia kuwa asilimia 67 ya wanufaika ni wanawake na watoto wa kike ambao tunaamini wataleta mabadiliko chanya kwenye jamii zao," amesema.

Meneja wa Kongani ya Kilombero kutoka Taasisi ya SAGCOT, Bw. John Nakei, amesema kuwa Taasisi yake itaendelea kutoa ushauri, kuwaunganisha na fursa za masoko, na kutoa elimu zaidi kwa wakulima katika mikoa hiyo ili kuwasaidia kuendesha shughuli hizo za kilimo kwa tija zaidi na kuwezesha uzalishaji endelevu wa chakula.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Ugani kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dkt. Kejeri Gillah, licha ya



kuwapongeza wadau katika utekelezaji wa mradi huo, ameshauri kuweka mkakati wa uendelezaji wa shughuli zilizofanywa kwenye mradi huo ili wakulima wengi zaidi wanufaike na mafunzo hayo.

Mkurugenzi wa VETA Kanda ya Nyanda za Juu, Bi. Susan Magani, amesema VETA inaendelea na jitihada mbalimbali za kuhakikisha mafunzo ya ufundi stadi yanawafikia wananchi wengi zaidi, hasa maeneo ya vijijini, na kwamba anaamini kuwa wakulima wengi zaidi nchini watanufaika na mafunzo hayo ili kuboresha shughuli zao.



Mradi wa Tajirika na Kilimo ulianza kutekelezwa mwaka 2018 kwa lengo la kujenga na kuimarisha ujuzi katika sekta ya kilimo kwa wakulima 2,200 na unatarajiwa kumalizika Desemba 2021.





VOCATIONAL EDUCATION AND TRAINING AUTHORITY
VETA
SKILLED LABOUR FORCE - THE FUTURE OF TANZANIA

WANAWAKE WANAWEZA



## VETA YAKABIDHI VIFAA VYA MILIONI 62 KWA VYUO BINAFSI

Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) kupitia VETA Kanda ya Kati imetoa vifaa vya kufundishia vyenye thamani ya Shilingi Milioni 62.8 kwa vyuo vya Ufundi Stadi vinavyomilikiwa na watu binafsi, Mashirika ya Dini na Mashirika ya Kijamaa.

Akikabidhi vifaa hivyo katika hafla iliyofanyika jijini Dodoma tarehe 3 Agosti, 2021, Mkurugenzi wa VETA Kanda ya Kati Bw. John Mwanja amesema uwezeshaji huo unalenga kuboresha utoaji wa mafunzo ya ufundi stadi katika kanda hiyo, kuongeza udahili na kuwezesha vyuo kuendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Amesema VETA inatambua mchango mkubwa unaotolewa na vyuo binafsi katika kuwapatia vijana ujuzi na hivyo imeona ni vyema kuviongezea nguvu vyuo hivyo ili viweze kujiimarisha katika kutoa mafunzo.

"Tunaamini kupitia vifaa hivi tulivyovitoa leo utoaji mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi utaenda kuboreka na hatimaye kuandaa vijana wetu ili waweze kuhitimu wakiwa na stadi mahiri zitakazowawezesha kujipatia ajira na kukuza uchumi," alisema

Naye Mratibu wa Vyuo vya Ufundi Stadi Kanda ya Kati, Bi Joyce Mwang'onda, alisema vifaa hivyo vimekuwa vikitolewa kwa awamu na kutaja vyuo vilivyonufaika kuwa ni Don Bosco VTC, St.Gabriel VTC, St.Ursula Ludochowaski, Sema VTC, na Veyula VTC.





Naye mwakilishi wa Mkuu wa Chuo cha Don Bosco Bw. Auson Ntoba alisema vifaa hivyo vitainua hamasa kwa wanafunzi kujifunza kwa vitendo zaidi .

Naye Mkuu wa chuo cha St. Ursula VTC Sista Josephina Mbori aliishukuru VETA kwa msaada huo wa vifaa na kuahidi kuvitumia vyema kutoa ujuzi kwa wanafunzi chuoni hapo.



# VETA YANG'ARA MAONESHO YA SABASABA 2021




Katika Maonesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (Sabasaba), yaliyofanyika kuanzia tarehe 28 Juni hadi 13 Julai 2021, VETA iliibuka Mshindi wa Kwanza katika Kundi la Uendelezaji Ujuzi. Maonesho hayo yalikuwa na Kaulimbiu ya, "Uchumi wa Viwanda kwa Ajira na Biashara Endelevu."





# CHUO KIPYA CHA VETA KUANZISHWA WANGING'OMBE

Wananchi wa Wilaya ya Wanging'ombe mkoani Njombe wanatarajia kuanza kupata mafunzo ya ufundi stadi katika Chuo cha VETA kinachotarajiwa kuanzishwa Wilayani Wanging'ombe katika mwaka wa masomo ujao.

Hayo yamebainishwa tarehe 4 Agosti, 2021 na Mkurugenzi Mkuu wa VETA, Dkt. Pancras Bujulu, alipotembelea na kukagua majengo na miundombinu katika Kijiji cha Ufwala, ambayo itakarabatiwa na kuboreshwa ili kukidhi mahitaji ya msingi ya chuo cha ufundi stadi.

Dkt. Bujulu amesema Chuo hicho kitaanzishwa katika majengo na miundombinu iliyokuwa ikimilikiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe kufuatia Halmashauri hiyo kukabidhiwa na Wakala wa Barabara nchini (TANROADS). Awali, majengo hayo yalitumiwa na Mhandisi Mkazi aliyesimamia ujenzi wa Barabara ya Nyigo-Igawa, mkoani Njombe.



Mwenyekiti wa Kijiji cha Ufwala kilipo Chuo hicho, Bw. Failos Ng'umbi, amesema kuwa wananchi wa kijiji chake wanasubiri kwa hamu kubwa kuanza kwa mafunzo Chuoni hapo.



Alisema mahitaji ni makubwa mno Wilayani humo, hivyo akaiomba VETA kuharakisha matayarisho, ili mafunzo hayo yaweze kuanza haraka iwezekanavyo. Mwenyekiti huyo amebainisha kuwa kijiji chake kiko tayari kutoa ardhi ya nyongeza kwa kadri ya mahitaji ya VETA kwa ajili ya kupanua Chuo hicho.





Kwa niaba ya Mamlaka, Mkurugenzi Mkuu alimshukuru Mwenyekiti na viongozi wengine waliohudhuria ukaguzi huo, wakiwemo Katibu wa Mbunge wa Jimbo la Wanging'ombe Bw. Erasto Danda, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Wanging'ombe (WEO) Bi. Beth Mangula na Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Ufwala (VEO) Bi. Irene Nungwi.

# MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

## ANUANI NA SIMU ZA OFISI ZA VETA ZA KANDA

| Na. | Ofisi za Kanda | Mikoa | Anuani |
|---|---|---|---|
| 1. | Kanda ya Kati | Dodoma, Singida, na Manyara | S.L.P 2084, Dodoma<br>Simu: 026 2322383<br>Nukushi: 0262324120<br>Barua pepe: vetacentral@veta.go.tz |
| 2. | Kanda ya Dar es Salaam | Dar es Salaam | S.L.P 40274, Dar es Salaam<br>Simu: 026 2862651<br>Nukushi: 026 2862651<br>Barua pepe: vetadsm@veta.go.tz |
| 3. | Kanda ya Mashariki | Pwani na Morogoro | S.L.P 1955, Morogoro<br>Simu: 023 4526<br>Nukushi: 023 4526<br>Barua pepe: vetaeastern@veta.go.tz |
| 4. | Kanda ya Ziwa | Mwanza, Mara, Geita na Kagera | S.L.P 1983 Mwanza<br>Simu: 028 2573013/4<br>Nukushi: 028 2573013<br>Barua pepe: vetalake@veta.go.tz |
| 5. | Kanda ya Kaskazini | Arusha, Kilimanjaro na Tanga | S.L.P 1738, Moshi<br>Simu: 027 2754468<br>Nukushi: 027 2754468<br>Barua pepe: vetanorth@veta.go.tz |
| 6. | Kanda ya Kusini Mashariki | Mtwara na Lindi | S.L.P 700, Mtwara<br>Simu:123 2333821 / 2333453<br>Nukushi: 023 2334078<br>Barua pepe: vetasoutheast@veta.go.tz |
| 7. | Kanda ya Kusini Magharibi | Mbeya, Rukwa, Songwe na Katavi | S.L.P 2498, Mbeya<br>Simu: 025 2504369/72<br>Nukushi: 025 2504370<br>Barua pepe: vetasouthwest@veta.go.tz |
| 8. | Kanda ya Magharibi | Kigoma, Tabora, Simiyu na Shinyanga | S.L.P 1218, Tabora<br>Simu: 026 26048990<br>Nukushi: 026 2604890<br>Barua pepe:vetawz@veta.go.tz |
| 9. | Kanda ya Nyanda za Juu | Iringa, Njombe na Ruvuma | S.L.P 818, Iringa<br>Simu: 026 2702351<br>Nukushi: 026 2700693<br>Barua pepe: vetahighland@veta.go.tz |



## Kwa mawasiliano na taarifa zaidi:

VETA Makao Makuu,
Plot No. 18, Central business Park (CBP)
Barabara ya VETA,
S.L.P 802,
DODOMA.

Baruapepe: info@veta.go.tz au pr@veta.go.tz
Simu: +255 755 267 489
Nukushi: +255 22 2863408
Tovuti: www.veta.go.tz

